**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

"Kilimani" Iringa Road,
S.L.P. 1175,
41101 DODOMA,
Barua Pepe: rbcdodoma@pccb.go.tz.
**TANZANIA.**

www.pccb.go.tz

**DODOMA – JANUARI 16, 2021**

# TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

MAHAKAMANI KWA KUSABABISHA HASARA YA YA SHILINGI 428,011,666/=

**Ndugu Wanahabari,**

Tunakutana kuwapatia taarifa za utendaji wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma kwa robo ya Oktoba hadi Desemba, 2020 kwa lengo la kuchochea mapambano dhidi ya rushwa.

**Kwanza**, Ufuatiliaji wetu wa fedha za umma, miradi ya maendeleo na kero za wananchi umewezesha kuokoa au kudhibiti jumla ya shilingi milioni mia mbili themanini na tatu laki tisa sabini na sita mia saba sitini na sita (**283,976,766/=)** pamoja na viwanja 14 na shamba moja la ekari 5. Fedha hizo ni mikopo umiza iliyorejeshwa kwa wananchi wanyonge; zilizolipwa kinyume na taratibu; madeni ya vyama vya akiba na mikopo (SACCOS); na mishahara hewa. Viwanja vimerejeshwa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa wananchi waliostahili lakini wakadhulumiwa na shamba limerejeshwa kwa Uhamiaji SACCOS.

**Pili,** ili kuwezesha Halmashauri kuongeza mapato ili ziweze kujitegemea, chanzo kimojawapo ni kodi ya ushuru wa huduma (service levy) ambapo ufuatiliaji wetu umebaini kwamba baadhi ya makampuni ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na maji hawalipi kodi hiyo na hivyo kuzifanya halmashauri kukosa mapato stahiki.

Kwa mfano tumebaini kwamba zaidi ya shilingi milioni mia tano (500,000,000/=) hazikulipwa na makampuni hayo kati ya mwaka 2017 na 2020. TAKUKURU kwa kushirikiana na TANROADS na DUWASA imeanza kufuatilia ili fedha hizo zilipwe na kuweka mfumo mzuri ambapo kodi hiyo itakuwa inalipwa moja kwa moja kila malipo yanapofanyika kwa makampuni.

**Tatu,** ili kukuza uungwaji mkono na jamii katika mapambano dhidi ya adui rushwa, TAKUKURU inatumia mbinu mbalimbali kuhamasisha ushiriki wa wadau na wananchi kwa ujumla katika mapambano hayo. Katika kipindi tajwa, tumefanya semina 75, maonesho 11 na mikutano 49 ya hadhara. Aidha, katika kuchochea vijana kushiriki mapambano hayo tumeimarisha klabu 165 za wapinga rushwa. Elimu hii imechangia kukuza uelewa wa wananchi katika kuzuia na hata kutoa taarifa za vitendo vya rushwa.

**Nne**, katika eneo la uchunguzi tumepokea jumla ya malalamiko 178 ya rushwa na makosa yahusianayo ambapo sekta zilizoongoza kulalamikiwa ni: Serikali za mitaa (asilimia 23); Mikopo umiza/sekta binafsi (asilimia 20); Ardhi (asilimia 14); Vyama vya siasa/uchaguzi (asilimia 6); Polisi (asilimia 6); na Afya (asilimia 6). Uchunguzi wa majalada 16 ulikamilishwa na mashauri 13 kufunguliwa mahakamani. Aidha, Mahakama ilitoa uamuzi wa mashauri 12 ambapo Jamhuri imeshinda 10 na kushindwa mawili.

**Tano**, Pamoja na shughuli nyingine katika robo ya Januari hadi Machi, 2021 tutaweka mkazo kuchunguza ubadhirifu wa fedha za umma hasa zinazotolewa kama mikopo kwa Taasisi, Vyama vya ushirika na watu binafsi na kufuatilia fedha za kodi ya ushuru wa huduma ambazo zilipaswa kulipwa na makampuni lakini hawakufanya hivyo kama tulivyoeleza hapo juu.

**Aidha**, tunawashikilia wanafunzi 13 wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) cha Jijini Dodoma kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya rushwa na udanganyifu wakati wa kufanya mtihani wa marudio (supplementary examination) wa somo la Applied Statistics II kwa mwaka wa tatu uliofanyika Novemba mwaka jana Chuoni hapo.

Uchunguzi wa awali umeonyesha kwamba wanafunzi hao, kwa kutumia rushwa, waliweza kurudia kufanya mtihani huo nje ya chumba cha mtihani na baadaye wakajaribu kuingiza karatasi za kujibia mtihani (examination booklets) kwenye mfumo rasmi lakini Chuo kikawabaini na kutupa taarifa. Pia tunawataka waliokuwa wanafunzi wa chuo hicho **Bw. Evarist Anthony Nyaki** na **Bw. Lameck Kawinga** kuripoti mara moja kwenye Ofisi zetu hapa Dodoma kwa ajili ya kusaidia uchunguzi wetu.

**Vilevile**, TAKUKURU mkoa wa Dodoma inaendelea na uchunguzi dhidi ya kampuni ya Geneva Credit Shop ya Mjini Kondoa inayojishughulisha na ukopeshaji baada ya kupokea malalamiko ya wananchi 30 ambao wanadai kupatiwa mikopo umiza na Kampuni hiyo. Uchunguzi wetu wa awali umeonyesha kwamba pamoja na kampuni hiyo kufanya biashara kwa zaidi ya miaka 25 lakini ilisajiliwa rasmi Oktoba, 2016 na hivyo haikuwa inalipa kodi. Tumebaini kwamba wengi wa wakopeshwaji ni watumishi wanaokaribia kustaafu na wamekuwa wakilipishwa riba kubwa sana kinyume na taratibu za nchi.

Kamati ya Usalama wilaya ya Kondoa ilifuatilia suala hili na kufanikiwa kukamata kadi za benki (ATM cards) zaidi ya 400 zikiwa zimeshikiliwa na mmiliki wa kampuni hiyo **Bw. Abubakary Idd Kinyuma** maarufu kama **Abubakary Mapesa** ambaye tunamtafuta na kumtaka kuripoti mara moja katika Ofisi zetu. Mfano, mmoja wa waliolalamika kwetu alikopeshwa shilingi 350,000/= lakini pamoja na kurejesha shilingi 4,600,000/=, alipostaafu mwaka 2018 alikamatwa na Bw. Mapesa na kutakiwa kurejesha shilingi milioni 35 zaidi. Aidha, imebainika kwamba Mfanyabiashara huyo amekuwa na tabia ya kuwaandikisha wadeni wake mikataba kwa nguvu na baadaye kuipeleka Mahakamani ili kuhalalisha madai yake.

**Pia**, tumemkamata raia wa Kenya **Bw. Alexander Kiema Mwikali** (42) ambaye anaishi Nkuhungu Jijini Dodoma akifanya kazi kama Mtaalam wa nyama wa Kampuni ya Alkafil kwa kosa la kutoa rushwa ya shilingi laki mbili (200,000/=) kinyume na kifungu cha 15 (1)b cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na rushwa namba 11/2007 kwa Mganga Mkuu wa Serikali **Prof. Abel Nkono Makubi** kama kishawishi ili ampatie cheti cha uthibitisho wa kutokuwa na ugonjwa wa Corona (Covid 19). Baada ya kuandaa mtego uliofanyika Ofisini kwa Profesa

Jijini Dodoma na kumnasa, Mtuhumiwa aliyetaka cheti hicho ili aweze kusafiri nje ya nchi alifikishwa katika mahakama ya Mkoa Dodoma na kufunguliwa shtaka ambalo alikiri na kutozwa faini ya shilingi laki tano (500,000/=) na pia Mahakama ikataifisha fedha aliyotoa kama hongo.

**Sita**, kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, keshokutwa tutamfikisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma **Bi. Severo Severin Mutegeki** (42) mkazi wa Ntyuka Jijini Dodoma ambaye alikuwa Mhasibu Msaidizi Mapato wa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) na kumfungulia shauri la uhujumu uchumi ambapo atashtakiwa kwa makosa matatu ya matumizi mabaya ya mamlaka kinyume na kifungu cha 31; Ubadhirifu kinyume na kifungu cha 28(a) vyote vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007; na kuisababishia Mamlaka hasara ya shilingi 428,011,666/= kinyume na Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 Marejeo ya mwaka 2019.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Dodoma umeonyesha kwamba kati ya Julai na Novemba, 2015, Mtuhumiwa alishindwa kuzingatia kanuni za fedha za DUWASA na kufuja sehemu ya maduhuli yaliyokusanywa badala ya kuyawasilisha benki.

**Mwisho,** tunawataarifu wananchi wa Mkoa wa Dodoma kwamba kila Jumanne ya kwanza ya mwezi tutakuwa na programu za kukutana nao katika maeneo yao ili kusikiliza kero za rushwa hivyo ni vyema waitumie fursa hiyo vizuri. Kwa miezi ya Februari na Machi, 2021 tutashirikiana na TANESCO kusikiliza kero za rushwa katika zoezi la kuwaunganishia wananchi umeme.

Pia tunawashukuru kwa kutupa ushirikiano na tunazidi kuwasihi kushiriki kivitendo kukataa vitendo vya rushwa. Rushwa hailipi.

**Imetolewa na:**

**Sosthenes Kibwengo**
**Mkuu wa TAKUKURU (M) Dodoma**